

**HALMASHAURI YA WILAYA KONDOA**  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

WILAYA YA KONDOA  
Fax/Simu 026 2360313  
E-Mail: [ded@kondoadc.go.tz](mailto:ded@kondoadc.go.tz)



Sanduku la Posta 1  
KONDOA

**TANGAZO LA KAZI (LINARUDIWA)**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya KondoA anawatangazia tena wananchi wote nafasi za kazi ya mkataba wa kipindi cha mwaka mmoja kwa wananchi wenye sifa waweze kujaza nafasi hizo.

Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatavyo:-

**1. MSAIDIZI WA HESABU (ACCOUNTS ASSISTANT): Nafasi 3**

***Majukumu:***

- (i) Kuandika na kutunza rejista zinazohusu shughuli za uhasibu
- (ii) Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha
- (iii) Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu za vituo vya kutolea huduma ya Afya.
- (iv) Kupeleka barua /nyaraka za uhasibu Benki
- (v) Kufanya usuluhishi wa masurufu, karadha, hesabu za Benki na amana.

***Mwombaji awe na sifa zifuatazo:-***

- (i) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)
- (ii) Awe amepata mafunzo ya cheti cha ATEC level III au foundation level kinachotelewa na NBAA au aliyefuzu mafunzo ya cheti (certificate) katika fani ya uhasibu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**N.B (Waombaji wenye sifa za stahada, shahada na Basic Certificates (NTA Level 4) wanajilishwa kutokuomba nafasi hizi kwa kuwa sifa zao si sahihi kwa mujibu wa muundo wa nafasi hizi)**

- (iii) Awe Raia wa Tanzania
- (iv) Awe na umri usiozidi miaka 45

**Vigezo na Masharti ya Jumla kwa waombaji:**

- (i) Mwombaji awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na serikali.
- (ii) Awe na umri na usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18
- (iii) Maombi yote yaambatanishwe na nakala ya cheti cha kuzaliwa, nakala ya cheti cha Taaluma, nakala ya Cheti cha kidato cha nne/sita, maelezo binafsi (CV), picha (passport size mbili) za hivi karibuni.
- (iv) Vyeti vyote vya Taaluma na kidato cha nne/sita ni lazima vithibitishwe na Hakimu au wakili anayetambulika na Serikali.
- (v) Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu, maombi yake hayatashughulikiwa.

Barua zote zitumwe kwa njia ya Posta, maombi yatakawasilishwa kwa mkono au barua pepe hayatafanyiwa kazi.

Barua zote zitumwe kwa njia ya Posta kupitia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P 01,

**KONDOA.**

**Tangazo hii limetolewa tarehe 25/09/2017 na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09/10/2017 saa tisa na nusu Alasiri.**



Abubakar A. Kuuli

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

**KONDOA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
KONDOA**